Africa Journal of Language Studies (AJLS)
Vol. 2 Issue 1 | [December] [2025] | [Page 43] – [Page 66]
Journal homepage: https://ajls.kab.ac.ug
ISSN: 3078-4301

# Uchanganuzi Amilifu-Zalishi Wa Miundo Ya Kimofolojia

Salim Sawe[1], Mosol Kandagor[2]

[1]Chuo Kikuu cha Kabianga
[2]Chuo Kikuu cha Moi,
Corresponding author: mosolkandagor@mu.ac.ke

**Article History:**
**Received:** 12 Mar 2025
**Accepted:** 05 Oct 2025
**Published:** 26 Dec 2025

**Maneno Muhimu**: Nyuklia, Satalaiti, Uamilifu, Uzalishi, Kategoria za kimofolojia

*This is an open access article under the CC-BY-NC-ND license*

**Ikisiri**
Makala hii ni uchanguzi amilifu-zalishi wa miundo ya kategoria za kimofolojia. Inachunguza utata unaotokea katika ufafanuzi wa dhana ya neno na aina za maneno katika Kiswahili. Utata huu unatokana na mitazamo tofauti ya wanasarufi kuhusu aina za maneno kama kategoria za kimofolojia, ambapo wengine wanabainisha aina saba, na wengine nane. Data inayochanganuliwa katika makala haya imekusanya mazungumzo ya Kiswahili sanifu kwa kutumia usampulishaji wakilishi wa kimakusudi. Nadharia Amilifu Zalishi (NAZ) inasisitiza uamilifu wa viambajengo katika kuunda miundo ya kisarufi, ikihusisha fonolojia, mofolojia, na sintaksia. Aidha, makala inaeleza kwamba neno linaweza kufasiliwa kwa njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na njia ya kiothografia, kifonolojia, kimofolojia, kisemantiki, na kisintaksia. Matokeo yanaonesha kuwa ubainishaji wa aina za maneno unapaswa kuzingatia uhusiano kati ya kategoria mbalimbali, na kwamba neno linaweza kuwa na maana tofauti kulingana na muktadha wa matumizi. Kwa hivyo, makala inatoa mchango mkubwa katika kitengo cha Isimu Fafanuzi na Isimu Nadharia.

## Abstract
*This paper presents a generative-transformational analysis of the structures of morphological categories. It examines the complexities that arise in defining the concept of word and the classification of word categories in Kiswahili. This ambiguity stems from differing linguistic perspectives regarding the morphological categorization of words, with some grammarians identifying seven categories and others eight. The data analyzed in the article were collected from standard*

*Kiswahili conversations using purposive representative sampling. The Functionalist-Generative Theory (FGT) emphasizes the productivity of morphemes in the formation of grammatical structures, encompassing phonology, morphology, and syntax. Furthermore, the article explains that a word can be defined in various ways including orthographically, phonologically, morphologically, semantically, and syntactically. The findings reveal that the classification of word categories should take into account the interrelationships among different categories and that a word may acquire different meanings depending on the context of use. Consequently, the paper makes a significant contribution to the field of Descriptive and Theoretical Linguistics.*

**Key Words:** Satellite, Nucleus, Functional, Generativity, Morphological Categories

## 1. Utangulizi

Uchanganuzi na ufafanuzi wa miundo ya maneno ya Kiswahili unaofanywa katika makala hii unaongozwa na nadharia amilifu zalishi ikiwa nadharia ya sarufi inayosisitiza uchambuzi wa miundo ya maneno inayokitwa kwenye nyuklia huru (mizizi) au miunganisho ya nyuklia tegemezi (mizizi) na satalaiti (viambishi). Msisitizo mwingine wa nadharia amilifu zalishi ni kwamba uzalishaji wa maneno huhusu uunganishwaji wa mofu zenye uamilifu wa kimuundo na kisemantiki. Hivyo basi, uchanganuzi wa miundo ya maneno ni sharti uoneshe viambajengo vya neno na uamilifu wa kila kiambajengo vile inavyoashiriwa kwa matumizi ya vielelezo tungo katika makala hii.

Uhakiki wa maandishi ya kisarufi inayohusu mofolojia ya Kiswahili unaashiria kutofautiana kwa wataalamu kuhusu uanishaji wa maneno. Mathalani, wanasarufi kama Nkwera (1989) na Kapinga (1983) wanadhihirisha aina saba za maneno ilihali watafiti kama Habwe na Karanja (2004) na Mgullu (1999) wanabainisha aina nane za maneno. Makala hii inasisitiza kuwa ubainishaji wa aina nane za maneno unachangia katika kuendeleza umataifa wa ufafanuzi katika Mofolojia ya Kiswahili. Hivi tutakuwa tukifanya vile inavyofanywa katika Mofolojia za lugha nyinginezo, kwa kufanya hivyo, tutatimiza usifabia unaolengwa na taaluma ya Isimu.

Ufafanuzi wa dhana ya neno unaotolewa katika makala hii kwa pamoja na uchanganuzi wa miundo ya maneno unaoonyeshwa utachangia kuendeleza Isimu Fafanuzi na Isimu Nadharia kwa Kiswahili. Ishara 'A' iliyotumiwa kwenye vielelezo kadha wa kadha vinavyojitokeza katika makala hii inarejelea 'Kiambishi' ambacho kinaweza kuwa cha awali au cha tamati.

## 2. Msingi wa Kinadharia

Kimsingi makala hii inachanganua miundo ya maneno kwa kuzingatia viambajengo


vinavyotumiwa kiuamilifu kuijenga kwa kuongozwa na Nadharia Amilifu Zalishi (NAZ). Nadharia hii ni modeli inayolenga kujenga vigezo vya kutazama Isimu kimawasiliano misingi fafanuzi inayotilia maanani mawanda yote ya taaluma ya Isimu. Nadharia hii inafaa kwa uchunguzi na uchanganuzi wa Fonolojia, Mofolojia, Sintaksia, Semantiki, Diskosi/Matini, Isimu jamii kwa kutilia maanani kwamba lugha ni chombo cha mawasiliano (Sawe, 2015; Sawe na Kipkosgei, 2017; Kandagor na Sawe, 2020).

Nadharia za awali zilisisitiza vipengele maalumu zaidi kama uamilifu (Bloomfield, 1933; Halliday, 1985), muundo, uzalishaji (Chomsky, 1965; 2005) na Isimujamii. Nadharia Amilifu Zalishi iliendelezwa kwa kutilia maanani mseto wa mawazo ya Sarufi Zalishi, Sarufi leksika, Isimu Amilifu, Umitindo, Isimu-Matini na hata Uchanganuzi Kilongo (Chomsky, 1965, 1993, 1995 & 2000; Halliday, 1985, Halliday na Matthiessen, 2004). Nadharia Amilifu Zalishi, inakiuka madai ya Chomsky kwamba nadharia ya Isimu inafaa kujikita kwenye uchunguzi na ufafanuzi wa "umilisi" na kuufafanua "utendaji wa kiisimu" kama matumizi halisi ya lugha yanayoathiriwa na uamilifu, mitindo, uhusiano wa lugha, jamii na miktadha. Nadharia hii inatilia maanani umuhimu wa akili katika uhifadhi wa sauti za lugha na mofu zinazotumiwa katika kuzalisha miundo ya silabi, miundo ya maneno na hata miundo ya sentensi kwa kuzingatia kanuni na ubunifu hadi tunapoweza kuzalisha usemi au matini zenye urefu utakaoweza kupitisha ujumbe unaolengwa kufanikisha mawasiliano.

NAZ inafafanua kwamba satalaiti na nyuklia huunganishwa akilini kama viambajengo ili kuunda neno kwa mujibu wa maana inayolengwa kuwasilishwa katika tukio kimawasiliano (Sawe na Mwamzandi, 2016; Kandagor na Sawe, 2019). Nyuklia ni kiini au kiambajengo kikuu cha muundo. Mzizi wa neno katika mofolojia hivyo basi ni nyuklia ya muundo unaozalishwa. Satalaiti nayo ni kitegemezi au kiambajengo chenye uamilifu wa kuijaliza nyuklia ya neno. Viambishi vikiwa vitegemezi (satalaiti) hutegemezwa kwenye nyuklia (mizizi) kwa kutegemea sifa za nyuklia na maana inayolengwa kupitishwa. Sensa za akili ya mtu anayejua lugha maalum zinatambua nyuklia ipi inajitosheleza kama neno na ipi inahitaji kuunganishwa na satalaiti ili iweze kuwasilisha maana. Sehemu ya ujuzi unaohifadhiwa akilini inahusu paradimu zinazoweza kukaliwa na satalaiti kama viambishi awali au vya tamati. Ujuzi huo huchochea sensa za akilini kutambua iwapo miungano ya nyuklia na satalaiti inazalisha maneno yenye maana. Iwapo msemaji atatambua kuwa hajazalisha neno ipasavyo, ataweza kujirekebisha au kuwarekebisha wengine.

**3. Kategoria za Kimofolojia**

Wanamofolojia kama vile Mgullu (1999), Habwe na Karanja (2004) na wengine wengi wamekuwa wakibainisha aina nane za maneno. Nadharia Amilifu Zalishi imeweza kuratibu aina hizo nane chini ya aina mbili kuu za maneno ambazo ni (i) maumbo ya kileksika na (ii) maumbo amilifu.




### 3.1 Maumbo ya Kileksika

Maumbo ya kileksika ni dhana inayotumiwa katika Nadharia Amilifu Zalishi kurejelea kategoria moja ya kimofolojia inayojumisha ***nomino*** na ***vitenzi***. Dhana hii inaonyesha kwamba maumbo yenyewe yana maana hata kabla hayajatumiwa katika sentensi (Sawe, 2007). Nadharia hii inadahili kwamba kitenzi kikiwa umbo la kileksika ni nyuklia ya sentensi hushirikiana na nomino (au kiwakilishi chake) inayokalia paradimu ya satalaiti ili kujenga muundo wa kisintaksia unaowasilisha maana.

Kwa mtazamo wa nadharia hii, maumbo ya kileksika kama ni mofu huru hayahitaji kuzanzuliwa (au kuchakatwa kisarufi akilini) ili huwa yanahifadhiwa akilini jinsi yalivyo. Hata hivyo, nomino kama 'mtu' na 'kitu' huwa tayari yanabeba viambishi vya nomino. Hii inamaanisha kwamba maumbo haya yanahifadhiwa yakiwa maneno wala sio kama mizizi na viambishi. Hata hivyo, nadharia hii imefafanua kwamba vitenzi huwa vinahifadhiwa akilini kabla hazijazanzuliwa zaidi ya kiwango cha shina (mzizi na kiishio). Viambishi vya awali na vya tamati huongezwa kwenye mzizi wakati tu wa kuunda sentensi. Haiwezi ikawa kwamba vitenzi huwa vimenyambuliwa bali vinanyambuliwa wakati mzalishaji wa sentensi anajua anataka kuzungumzia kitendo kilichofanywa ili na nani ndipo kuwe na viambishi vifaavyo vya kiima, vya njeo, vya hali na vya yambwa. Lengo la mzungmzaji huathiri uteuzi wake wa vitenzi na vijenzi vigine vya kifungutenzi.

### 3.2 Maumbo Amilifu

Aina sita za maneno (ambazo ni ***vivumishi, viwakilishi, vihusishi, vihisishi*** na ***Viunganishi***) zimetengwa chini ya kategoria hii kulingana na nadharia hii. Nadharia hii inasisitiza kwamba Mofolojia haipaswi kuyaanisha maumbo amilifu kwa daraja moja na maumbo ya kileksika. Hii ni vile vivumishi vina uamilifu wa kueleza zaidi kuhusu nomino huku viwakilishi

vikitumika tu kiuamilifu kama vibadala vya nomino. Vivumishi navyo vina uamilifu wa kuonyesha uhusiano uliopo baina ya nomino moja na nyingine kwa mujibu wa mahali. Vihisishi ni faridi zenye uamilifu wa kudhihirisha hisia katika muundo. Hatimaye, viunganishi ni viambajengo vyenye uamilifu wa kuambatanisha vipashio vya kimofolojia vinavyotumiwa kujenga miundo ya kisintaksia.

Uteuzi na unganishwaji wa maumbo ya kileksika na ya kiuamilifu hudhibitiwa na mikuku ya kisarufi na kanuni za kifonolojia, kimofolojia na za kisintaksia. Uteuzi na uunganishaji huo unaodhibitiwa rejista ya mawasiliano, muktadha, lengo na valensia hufanywa mara moja pasipo kuwa na nafasi ya kufanya mageuzi kinyume na ilivyodaiwa na Chomsky katika nadharia yake ya Sarufi Geuza Maumbo Zalishi (Chomsky, 1965; 1993).

## 3.3 Dhana ya Neno

Dhana ya neno imeweza kuelezewa na wanaisimu kadha wa kadha kama vile Mathews (1994), Katamba (1993), Mgullu (1999) pamoja na Habwe na Karanja (2004) miongoni mwa wengine. Fasili za wataalamu hao, zinadokeza kuwa neno ni mfululizo wa herufi unaozungukwa na nafasi tupu lakini usiokuwa na nafasi tupu katikati, ni kipashio kidogo huru cha kisarufi chenye maana katika lugha neno. Sehemu ifuatayo inaonyesha fasili mbalimbali za wanaisimu kuhusu maana ya 'neno'.

### 3.4 Fasili ya Kiothografia ya Neno

Neno kwa misingi ya kiothografia ni umbo linalolobeba maana na ambalo limeandikwa kwa herufi halisi. Umbo lolote lenye muungano wa alfabeti za konsonanti na vokali usioibua maana kwa hivyo si neno hata kama litaandikwa kwa herufi chache au nyingi. Ufafanuzi huu wa neno unatatiza kwa vile inahusishwa na mifumo ya kiothografia au maandishi tu.

Neno linaweza kuelezewa kama ishara ya kiothografia inayoandikwa kwa kuunganisha herufi kwa namna ambavyo kutakuwa na nafasi baina ya ishara (neno) moja na ishara nyingine (neno). Hii inadhihirisha kwamba kuunganishwa kwa maneno mawili kwa namna ambavyo hakuna nafasi kati yao kunaonyesha kugeuzwa kwao kuwa neno moja. Mjadala muhimu unaopaswa kuendelezwa zaidi kuhusu muundo wa neno katika Mofolojia ni ule unaohusu *iwapo hatupaswi kabisa kuwa na nafasi katikati ya umbo tunalolirejelea kama 'neno'*. Kwa mfano, Sociolinguistics linafaa kuwakilishwa likiwa na nafasi kama **Isimu Jamii**, au bila nafasi katikati kama **Isimu-Jamii** au **Isimujamii**. Maneno mengine yanayochukua mwelekeo huo ni pamoja na askari kanzu, askari jela, askari polisi na bata mzinga ambayo ingawa yanashirikisha maumbo mawili mawili, kwa pamoja yanarejelea dhana moja moja.

Upungufu wa mkabala huu wa kiothografia hususan unatokana na kule kujifunga kwake kwa lugha andishi huku ukipuuza uhalisia kwamba maneno hutumika pia katika usemi au mazungumzo.

### 3.5 Fasili ya Kimofofonolojia ya Neno

Kwa mkabala huu, neno linaweza kufafanuliwa kama umbo la kimofofonolojia linaloundwa kwa kuunganisha idadi mahususi ya fonimu kwa mpangilio maalumu. Mpangilio huo wa fonimu hujenga silabi zinazotamkwa kwa kutilia maanani elementi za mkazo, wakaa na toni ili kuibua maana inayolengwa kwa kutegemea mfumo lugha unaotumiwa na mzugumzaji. Kwa misingi hii, neno ni kipashio cha kimofofonolojia kinachoundwa kwa fonimu moja au zaidi. Kwa mfano, neno moja linaweza kutofautiana na neno lingine kwa sababu ya toni au wakaa unaotumiwa katika neno linalozalishwa vile inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

Mifano ya wakaa:

| Neno | | Unukuzi | | Maana |
|---|---|---|---|---|
| Bidi | - | /bidi/ | - | Hitajika |
| Bidii | - | /bidi:/ | - | Jitihada |

Mifano ya toni (kutoka Kikipsigis):

| Kipsigis | | Kiswahili |
|---|---|---|
| Moét | - | Hakukua |
| Moet | - | Tumbo |
| Moèt | - | Kidonda |

Tukichanguza mfano wa Kikipsigis uliotolewa hapa juu, tunagundua kuwa neno linaweza kuwa umbo linaloundwa kwa fonimu moja au msururu wa fonimu unaobeba maana. Umbo linalozalishwa kwa fonimu moja au kwa kuunganisha fonimu hivyo ni faridi ya kiisimu inayojitosheleza kama umbo la kuwasilisha maana. Umbo lisilojitosheleza kuwasilisha maana kamili kwa hivyo si neno.

Aidha, kwa mtazamo wa makala hii, neno linaweza kufasiliwa kama tukio la kimofofonolojia linaloundwa kwa silabi moja au zaidi. Tukio au umbo hilo huwa na mkazo mmoja unaowekwa kwenye silabi mahususi kwa kutegemea kanuni za kimofofonolojia zinazotawala mfumo lugha unaohusika. Kubadilishwa kwa nafasi ambapo mkazo unawekwa katika neno kutaweza kubadilisha aina na maana ya neno litakalozalishwa. Kwa mfano, kwa kutegemea mahali ambapo mkazo unawekwa kwenye neno la Kiingereza ‘produce’ linaweza kuibuka kama kitenzi chenye maana ya ‘kuzalisha’ au likaibuka kama nomino yenye maana ya ‘mazao’. Vivyo hivyo, umbo la Kiswahili ‘barabara’ linaweza kutamkwa kama nomino [pale mkazo utakapowekwa kwenye silabi ya pili kutoka **mwisho wa neno**] kwa maana ya ‘njia’ au kama kielezi [pale mkazo utakapowekwa kwenye silabi ya pili kutoka **mwanzo wa neno**] kwa maana ya ‘shwari’ kwa kutegemea mahali ambapo mkazo utawekwa kwenye fungu zima la silabi. Maumbo ya aina hii yataweza kuhesabiwa kama maneno yanayotofautiana kwa sababu mikazo yao itakuwa imekalia paradimu zinazotofautiana.

Mkabala huu hata hivyo hautoshelezi ufafanuzi wa maneno yote yanayotumiwa katika lugha. Hii ni kwa vile lugha ina baadhi ya maneno yanayoundwa kwa silabi moja pekee. Mkazo hauwezi kubadilishwabadilishwa katika maumbo hayo. Hii inaonyesha kuwa sehemu ya

umilisi wa mtu mjua lugha yake ni ule wa kujua ataunda silabi kwa kuunganisha fonimu vipi na ataweka mkazo vipi kwenye silabi atakazozalisha ili aweze kujenga maumbo yenye maana anayolenga kwa ajili ya kufanikisha mawasiliano.

### 3.6 Fasili ya Kimofolojia ya Neno

Neno ni kipashio cha kimsingi katika uchambuzi wa kimofolojia. Kwa fasili ya kimofolojia, neno ni kipashio cha kiisimu kinachoundwa kwa mzizi mmoja au zaidi. Baadhi ya maneno yanaundwa kwa mofu huru lakini yale yanayoundwa kwa mofu tegemezi ni sharti yashirikishe viambishi ama awali au tamati. Neno linaloundwa kwa kutumia mbinu ya mwambatano ndilo linalojengwa kwa zaidi ya mzizi mmoja kama vile mwanasiasa [[mw] + [ana] + [siasa]]. Maneno machache mno yanaweza kuundwa kwa kuunganisha mizizi mitatu au zaidi katika lugha nyingi za binadamu. Mintarafu ya Sawe (2015), huenda hilo linatokana na ugumu wa kuchakata maumbo ya aina hiyo akilini.

Neno hurejelewa pia kama leksimu katika uchanganuzi wa kiisimu ndiposa neno linaanika vilevile kama faridi ya kileksika inayochunguzwa katika taaluma ya lugha. Neno linachukuliwa kama faridi dhahania ya kileksika inayosheheni maana. Faridi hii inaweza kutamkwa au kuandikwa (Crystal, 1980). Wanamofolojia hawajabainisha iwapo leksimu zinazojitokeza kama homonimu na homografu kama paa, kaa, barabara na nyingine nyingi zinawakilisha neno moja moja au maneno tofauti.

Kwa mtazamo wa makala hii, neno ni umbo la kimofolojia limalojisimamia peke yake na ambalo kategoria yake ya kimofolojia imaweza kubainishwa. Hii inamaanisha kwamba kategoria ya kila kipashio kinachorejelewa kama neno inaweza kudhihirishwa kama ni nomino, kitenzi, kihusishi, kivumishi, kiunganishi, kihisishi, kielezi au ni kiwakilishi. Maumbo yoyote yanayoweza kubainika kama maneno yanaweza kuainika ndani ya kategoria moja kati ya hizi kategoria nane za kimofolojia.

### 3.7 Fasili ya Kisemantiki ya Neno

Wanaisimu vilevile wameweza kufafanua maana ya 'neno' kwa kuzingatia uamilifu wake wa kuwasilisha maana. Ufasili wa dhana hii katika mkabala huu husisitiza maana kwa kudai kuwa neno ni lazima liwe na maana. Neno ni kipashio kidogo cha lugha chenye maana moja au zaidi. Hili ni umbo dogo huru ambalo haliwezi kugawika zaidi kuwa vipashio vidogo vinavyoweza kujisimamia huku vikileta maana (Mdee, 2010; Bloomfield, 1933). Baadhi ya maneno huwa na maana dhahiri hata kabla hayajatumiwa kuunda sentensi lakini maana za maneno mengine ambayo ni mofimu amilifu kama viunganishi hubainika pale yanapotumiwa tu kwenye sentensi. Kulingana na Nadharia Amilifu Zalishi, 'neno' ni kipashio kinachochangia maana katika sentensi hata ingawa maana inayoweza kutokea katika sentensi ni tofauti na maana za maneno yaliyotumiwa.

Neno ni umbo la kimofosemantiki linalobeba dhana au fahiwa ya kawaida au kitaaluma ndiposa maneno yanaweza kuanishwa kama msamiati na istilahi. Kila neno ni ishara ya

kisarufi ambayo ikitamkwa au ikiandikwa inawakilisha mofimu moja au zaidi katika akili za mtu anayejua lugha. Hii inamaanisha kwamba kila neno huwakilisha maana fulani katika akili za watu wanaoitumia lugha husika. Haiwezekani kutumia mfumo-ishara-amilifu wa kimaana iwapo maumbo (maneno) yenyewe hayawakilishi maana sawa katika akili za wasimbaji na wasimbuaji.

**3.8 Fasili ya Kisintaksia ya Neno**

Mkabala huu huona neno kama umbo la kisarufi lenye uamilifu wa kimuundo. Mkabala huu unatazama neno mintarafu ya matumizi yake kama kiambajengo kinachotumiwa katika ujenzi wa sentensi (Katamba, 1994). Neno likishiriki kama kiambajengo cha sentensi linaweza kuibua uamilifu wa lugha kama wa kueleza, kujieleza, kuburudisha, kufariji, kushawishi, kutangaza, kuarifu, kuamrisha, kukejeli na kurekebisha. Isitoshe, matumizi ya neno katika sentensi yanaweza kudhihirisha dhima za thita kama za kubainisha mtenda, mtendewa, kitumizi, malighafi, matokeo, lengo na vishamirishi ambazo haziwezi kudhihirishwa na neno lolote kiupweke kabla ya kutumika katika sentensi. Kwa mfano:

Kwa kurejelea kategoria za virai, neno linaweza kufafanuliwa kama kipashio cha kisarufi kinachoweza kushiriki katika ujenzi wa kirai kama kipashio kikuu au kiambajengo kifuasi. Mathalani, nomino ni neno kuu katika kirai nomino huku kitenzi kikiwa kiambajengo kikuu cha kirai kitenzi. Neno kwa hivyo ni kiambajengo cha kisintaksia kinachoweza kushirikiana na viambajengo vingine kwa kuzingatia ruwaza au kanuni za kisintaksia za lugha zinazotumiwa. Neno kama kategoria ya kimofolojia kwa hivyo linafaa kwa uchanganuzi wa kategoria za kisintaksia kama vile virai, vishazi na sentensi.

**3.9 Fasili ya Kilongo ya Neno**

Matumizi ya ‘neno’ katika mawanda yanayofungamana na Uchanganuzi wa Kilongo au Uchanganuzi wa Matini unaashiria kwamba faridi hii inaweza kutumiwa kwa misingi ya kipragmatiki katika miktadha maalum kama ya dini. Kwa mfano, kwenye sajili ya dini, Biblia inarejelewa kama ‘neno’ la Mungu, mahubiri yanaweza kurejelewa kama ‘neno’ wala sio ‘maneno’. Mhubiri anaweza kurejelewa kama mnenaji wa neno. ‘Neno’ katika sajili hiyo kwa kurejelea katika matini ya Yohana 1: 1-3 linamrejelea Yesu kwa jinsi ifuatayo:

> Hapo mwanzo Neno lilikuwepo (ikimaanisha Yesu alikuwepo mwanzoni), kwamba Neno (Yesu) alikuwako kwa Mungu Baba na Neno (yaani Yesu) alikuwa Mungu. Vyote viliumbwa kwa huyo Yesu (Neno) na bila Yeye vyote vilivyoundwa havingefanyika’.

Yohana 1: 1-3 *[Fasiri ya Kilongo kwa Kuzingatia maelezo kwenye muktadha huo wa Biblia]*

Matumizi ya neno katika mfano huu unapata maana yake kutokana na muktadha na

hayaashirii hasa umbo linaloundwa kwa fonimu au silabi zenye mkazo mmoja ila yanarejelea uhalisia unaoeleweka katika muktadha husika wa kipragmatiki.


## 4. Uchanganuzi Amilifu-Zalishi wa Muundo wa Neno


Uchanganuzi huu unazingatia misingi ya Nadharia Alimifu Zalishi kwamba miundo ya maneno hupaswa kuchambuliwa kwa kuzingatia uamilifu wa kila kiambajengo kinachobainishwa. Nadharia hii huchanganua muundo kiuamilifu kwa kuzingatia uamilifu wa kisemantiki wa viambajengo vinavyojenga mofu inayowakilishwa akilini mwa msikilizaji asilia. Hii inamaanisha kwamba mofimu zinazowakilisha mofu zinabainishwa kama faridi amilifu zinazofaa kwa uchanganuzi wa miundo ya maumbo ya kimofolojia. Kwa sababu hii, vielelezo miundo vinavyotumiwa katika uchambuzi wa miundo ya maneno katika sehemu zifuatazo zinatumia ishara kama $A^{Udhahania}$, $A^{Njeo}$, $A^{Hali}$, $A^{Kirejeshi}$ na $A^{Kiishio}$. Hapa ishara ‘A’ inawakilisha Kiambishi.


$A^{Udhahania}$ inaashiria mofimu ambayo ni kiambishi cha udhahania. $A^{Njeo}$ inaashiria mofimu ambayo ni kiambishi cha njeo kama wakati uliopo {na}, ujao {ta} au uliopita {li}. $A^{Hali}$ inaashiria mofimu ambayo ni kiambishi cha hali kama hali timilifu {me}, hali ya mazoea {hu} au hali ya masharti {nge}. Uchanganuzi wa **kiuamilifu-zalishi** wa kategoria kadha za kimofolojia ambazo ni nomino, kitenzi, kielezi na kivumishi unafanywa katika sehemu ifuatayo:


***Miundo ya Nomino***


Ifuatayo ni mifano ya nomino za Kiswahili na namna ambavyo twaweza kuchanganua nguzo za nadharia amili zalishi.





E
A udhahania
V
Satalaiti
Nyuklia
[u-]
[-choyo]



Utu
N
A udhahania
Mzizi
Satalaiti
Nyuklia
[u-]
[-tu]


Mtu
N
A^Ngeli
Mzizi
Satalaiti
Nyuklia
[m-]
[-tu]



Jitu
N
A^Ngeli
Mzizi
Satalaiti
Nyuklia
[ji-]
[-tu]



Watu
N
A^Ngeli
Mzizi
Satalaiti
Nyuklia
[wa-]
[-tu]


Kichapo





Kifuniko




Mlevi
N
A Ngeli
T
Mzizi
A Kiishio
Satalaiti 1
Nyuklia
Satalaiti 2
[m-]
[le(w)-]
[-i]



Mwimbaji
N
A Ngeli
T
Mzizi
T
A Kiishio
A Kinominishi
Satalaiti 1
Nyuklia
Satalaiti 2
Satalaiti 3
[mw-]
[-imb-]
[-a-]
[-ji]

Muundo wa nomino-ambatani unaweza kuundwa kwa nomino ($N^1$) [mcheza] ambayo imeunganishwa na nomino nyingine ($N^2$) [kamari] kama ufuatao. Muundo wa nomino ya kwanza ($N^1$) [mcheza] hata hivyo umeundwa kwa kukiunganisha kiambishi cha ngeli 'm' kwa kitenzi 'cheza'.




Kielelezo cha muundo kifuatacho kinaonyesha mfano wa muundo wa nomino-ambatani 'mwanasarufizalishi' ulioundwa kwa kuteua na kuunganisha nomino tatu ($N^1$) [mwana], ($N^2$) [sarufi] na ($N^3$) [zalishi].

Mwanasarufizalishi




**4.1 Miundo ya Vitenzi**

Kitenzi kimeelezewa na Massamba (2004) kama kipashio cha kisarufi kinachohusu tendo lililofanyika, linalofanyika na au litakalofanyika. Ufafanuzi huo hautenganishi njeo na kitendo. Swali muhimu linaloibuka kutokana na ufafanuzi wao ni iwapo kuna uwezekano wa kutenganisha kitendo na njeo katika ufafanuzi wa kitenzi. Ufafanuzi huo hata hivyo, kwa mtazamo wa makala hii, haujumuishi vitenzi vingine kama vitenzi vitamaushi, vimilikishi na vishirikishi.

Kulingana na makala hii, kitenzi ni kipashio chochote cha kimofosintaksia ambacho kitaibuka kama neno kuu la kirai kitenzi; ni faridi kuu katika kiarifa cha sentensi na ni kipashio kinachoweza kukalia paradimu inayokaliwa na kitenzi kingine katika sentensi.

Kwa kuzingatia mwongozo wa Nadharia Amilifu Zalishi, makala hii inabainisha **satalaiti** kadhaa zinazoshiriki katika ujenzi wa miundo ya vitenzi vya Kiswahili: Kwanza, inabainisha kwamba kipashio cha kimsingi kwenye muundo wa kitenzi ni **nyuklia** au **mzizi**. Pili, inadai kuwa mzizi ni viambajengo vikuu vya kileksika ambavyo vina uamilifu wa kuwakilisha maana ya kimsingi.


Tatu, viambishi vya upatanisho ni vijenzi vingine muhimu vya kiuamilifu vinavyounda **satalaiti** ya muundo wa kitenzi cha Kiswahili. Viambishi vipatanishi hivyo ni vya aina mbili: viambishi vya upatanisho wa kiima na viambishi vya upatanisho wa yambwa. Viambishi vya upatanishi vyenyewe huathiriwa na sifa za nomino inayorejelewa kwenye kiima au yambwa

kwa misingi ya ngeli na idadi.

Nne, viambajengo vingine vinavyojenga **satalaiti** za muundo wa kitenzi cha Kiswahili ni mofu za nafsi, za njeo na hali. Mofu za njeo hushirikisha za wakati uliopita, uliopo, ujao na wakati usodhahiri. Mofu za hali ni pamoja na zile za hali timilifu, hali ya mazoea na hali ya masharti. Mofu hizi hutumiwa kama viambishi awali vinavyotokea kabla ya mizizi ya vitenzi.


Tano, viambishi virejeshi (vya O-rejeshi) na viambishi vijirejeshi huweza kutumiwa kama viambishi vya awali au vya tamati katika miundo ya vitenzi vya Kiswahili. Hii inamaanisha kuwa vinaweza kuunda **satalaiti tangulizi** au **satalaiti tamatishi**. Sita, viambishi tamati vya mnyambuliko ni viambajengo vingine vya lazima katika uzalishaji wa muundo wa kitenzi cha Kiswahili. Hivi viambishi hujenga satalaiti zenye uamilifu wa kubainisha kauli au hali za vitenzi.


Saba, uzalishwaji wa kitenzi unaweza kujumuisha **satalaiti** zenye uamilifu wa kipekee kama viambishi tamati vya kubainisha hali ya wingi wa nafsi ya pili kama katika kitenzi ondokeni ambapo kuna mofu mzizi {ondok-} na mofu ya kubainisha wingi {-eni}. Viambishi vya wakati maalum na mahali maalum {-po} huweza kutumika vilevile kama kiambishi tamati katika uzalishaji huo wa muundo wa kitenzi cha Kiswahili.




Satalaiti 1 Satalaiti 2 Satalaiti 3 Nyuklia Satalaiti 4

[a-] [-li-] [-ku-] [arif-] [-u]









***Miundo ya Vielezi***







**4.2 Miundo ya Vivumishi**

Kivumishi ni umbo la kimofolojia linalotoa maelezo zaidi kuhusu nomino pale litakapotumiwa katika sentensi. Umbo hili hushirikiana na nomino katika ujenzi wa kirai nomino. Vivumishi ni vipashio vya kimuundo vyenye uamilifu wa kutoa maelezo zaidi


kuhusu nomino katika sentensi za lugha. Kwa misingi hii, umbo lolote linalotumika kama kivumishi haliwezi kujitokeza pasipokuwa na nomino au hata mbali na nomino. Ingawa kila kivumishi kina muundo wa ndani unaoweza kuchanganulika kimofolojia, hakiwezi kubainika pweke kama kivumishi ila tu kwenye matumizi.

Mifano ifuatayo (i) mpaka (iv) ni vivumishi vyenye asili ya kibantu na vimeonyesha ruwaza zenye mizizi inayotanguliwa na viambishi vya ngeli za nomino. Mifano yenyewe inaashiria kuwepo kwa mabadiliko ya kimofofonolojia ambayo yanaashiriwa kwa sababu ya tofauti katika umbo linalotamkwa (n(y)eusi) na (ki-eusi) na mofu zinazoashiriwa kwenye kielelezo tungo badala ya nyeusi na cheusi. Mifano (v) na (vi) ni ya vivumishi 'safi' na 'hodhari' vilivyokopwa kutoka Kiarabu ambavyo vinatumia mizizi isiyoambatanishwa viambishi vya awali.


[i]





[ii]



[iii]


Cheusi
V
A^Ngeli
Mzizi
Satalaiti
Nyuklia
[ki-]
[-eusi]


[iv]


Nzuri
V
A^Ngeli
Mzizi
Satalaiti
Nyuklia
[n-]
[-zuri]

[v]



Safi
V
Mzizi
Nyuklia
[safi]

[vi] hodhari





Baadhi ya miundo ya vivumishi viidadi vya Kiswahili inajengwa kwa mofu huru huku mingine ikijengwa kwa mizizi inayoambatanishwa na viambishi vya ngeli. Vivumishi vya akisami kama vile robo, nusu na theluthi ni mofu huru kwa kuwa havichukui viambishi vya ngeli. Vipo vivumishi vya kubainisha idadi vinavyorejelewa kama vivumishi vya pekee kama vile -ote na -o-ote. Vile inavyoonekana katika vielelezo vitatu vifuatavyo, vivumishi vya idadi vinavyobainisha idadi kamili kama vile tatu, moja na nane huchukua viambishi vya ngeli.


[i] Wanne




[ii] Vitano



[iii]




Miundo ya vivumishi viashiria hujengwa kwa mofu ya kuashiria {h-} ambayo inaambatanishwa na irabu inayotangamana na irabu inayotokea kwenye kiambishi cha ngeli. Kwa sababu hii, mofu {h} inaunganishwa na ‘a’ iwapo kivumishi kiashiria kinahusisha ngeli yenye ‘a’ kwenye umbo lake, ikaunganishwa na ‘u’ iwapo kivumishi kinahusisha ngeli yenye ‘u’ kwenye umbo lake na ikaunganishwa na ‘i’ iwapo kivumishi kinahusisha ngeli yenye ‘i’ kwenye umbo lake. Ruwaza hizi zinaashiria kuwa uteuzi wa irabu hutegemea mtangamano wa irabu katika neno litakaloundwa kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

irabu iliyonakiliwa kutoka irabu ya ngeli

a) H+**u**+**u** = huu
b) H+**i**+**i** = hii
c) H+**a**+w**a** = hawa
d) H+**i**+z**i** = hizi
e) H+**a**+y**a** = Haya
f) H+**i**+k**i** = Hiki
g) H+**u**+m**u** = Humu

Mifano (a) – (g) inaashiria kutangamana kwa ‘u’ na ‘u’, ‘i’ na ‘i’ na ‘a’ na ‘a’ katika ujenzi wa miundo ya maneno haya ambayo yanaweza kutumika kama vivumishi iwapo vitaeleza zaidi kuhusu nomino au kama viwakilishi iwapo vitatumika kama vibadala vya nomino. Hii inaashiria kwamba maumbo haya si vivumishi kwa sababu ya viumbile vyao ila kutokana na matumizi.

**5. Hitimisho**

Kwa kuhitimisha, katika kufasili dhana ya neno ni vyema kuzingatia vigezo vyote vya kisarufi kama vile othografia, fonolojia, sarufi, maana na lekisika ili kupunguza changamoto zinazojitokeza katika kufasili dhana hii kama ilivyojibainisha hapo juu. Hivyo, kulingana na vigezo tajwa hapo juu dhana ya neno yaweza kufasiliwa kama kipashio cha lugha kilichojengwa na vipande sauti mbalimbali vya matamshi, chenye maana aidha ya kilekisika au ya kisarufi, kinachoweza kujibainisha kimaandishi na kimatamshi na kuwa na uwezo wa kuchukua sifa mbalimbali kinapokuwa katika muktdha wa matumizi.

Makala hii imehitimisha kwamba uchanganuzi wa miundo ya maneno unafaa kufanywa kwa kuzingatia nguzo za nadharia amilifu-zalishi ambapo seti za nyuklia na satalaiti huteuliwa na kuunganishwa. Nyuklia huru hazihitaji kuunganishwa na satalaiti. Nyuklia hubeba maana za kimsingi katika miundo ya kimofolojia inayoundwa na satalaiti husheheni maana amilifu. Miundo ya aina mbalimbali za maneno huweza kuchanganuliwa. Nomino na vitenzi ni mofu za kileksika huku vivumishi, viwakilishi, vihusishi, vihisishi na viunganishi vikiwa mofu amilifu zinazohitaji kuunganishwa na mofu zingine ili maana zao ziweze kubainika.

**Marejeleo**

Bloomfield, L. (1933). *Language.* New York: Henry Holt.

Chomsky, N. (1965). Aspects of the Theory of Syntax. Cambridge, Massachusetts: MIT Press.

Chomsky, N. (1993). "A Minimalist Program for Linguistic Theory" Katika K. Hale na S. Jay (Wah.). The View from Building 20: Essays in Honor of Sylvain Brombeger. Cambridge, Massachusetts: MIT Press. Chomsky, N. (1995). The Minimalist Program. Cambridge: MIT Press.

Chomsky, N. (2000). New Horizons in the Study of Language and the Mind. Massachusetts: MIT Press.

Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Halliday, M. & Matthiessen, M. (2004). An Introduction to Functional Grammar. London: Arnold Publishers.

Halliday, M. (1985). An Introduction to Functional Grammar. London: Edward Arnold.

Kandagor, M. na S. Sawe (2020). Athari za Valensia ya Kitenzi katika Usarufi wa Miundo ya Kiswahili Jarida la CHALUFAKITA, JUZ. NA. 2

Kandagor, M. na Sawe, S. (2019). Muwala katika diskosi za wingi-lugha. JAKIIKI. 1, 80-90.

Kapinga, M. (1983). Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu. Dar es Salaam: TUKI.

Katamba, F. (1993). *Morphology*. London: MacMillan Press Ltd.

Massamba, D. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es salaam: TUKI

Mdee, S. (2010). *Nadharia na Historia ya Leksikografia*. Dar es Salaam: TUKI.

Mgullu, R. (1999). Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia. Longhorn Publishers

Nkwera, F.V.M. (1989). *Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Printpak.

Sawe, S. (2015). Mshikamano na Muwala katika Diskosi za Kiwingi-lugha: Hali katika Vyuo Vikuu Nchini Kenya. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Laikipia.

Sawe, S. na Kipkosgei, A. (2017). A Case of Unmarked Register in Mathematical Linguistics. Ellixir. 12, 26-30.